RIPOTI YA UTAFITI

# Mfumo wa mbegu unaosimamiwa na mkulima wilaya za Morogoro na Mvomero, Tanzania: Utajiri wa wakulima wadogo usiothaminiwa




african centre for biodiversity

kituo cha afrika cha bioanuwai

www.acbio.org.za

MVIWATA

SAT Tanzania Sustainable Agriculture

Mnamo Aprili 7, 2015 Kituo cha Afrika cha Usalama wa Kibaiolojia kilibadilisha jina lake rasmi na kuitwa Kituo cha Afrika cha Bioanuwai (ACB). Mabadiliko haya ya jina yalikubaliwa kupitia mashauriano ndani ya ACB ili yaakisi kupanuka kwa wigo wa kazi yetu katika kipindi cha miaka michache iliyopita. Machapisho yote ya Kituo cha Afrika cha Bioanuwai kabla ya tarehe hii yatabaki chini ya jina la zamani la Kituo cha Afrika cha Usalama wa Kibaiolojia, na kinapaswa kuendelea kufanyiwa marejeo kama hivyo.

Bado tuna dhamira ya kubomoa ukosefu wa usawa katika mifumo ya chakula na kilimo katika Afrika na imani yetu katika haki za watu za kupata chakula chenye lishe na stahiki kitamaduni, kilichozalishwa kupitia njia zilizo sahihi kiekolojia na endelevu, na haki yao ya kuainisha mifumo yao wenyewe ya chakula na kilimo.

© Kituo cha Afrika cha Bioanuwai
www.acbio.org.za
S.L.P. 29170, Melville 2109, Johannesburg, Afrika Kusini.
Simu: +27 (0)11 486 1156

Ubunifu na mpangilio: Adam Rumball, Sharkbuoys Designs, Johannesburg
Picha kwenye jalada: Vanessa Black

## Shukrani

Kituo cha Afrika cha Bioanuwai (ACB) kinatambua na kushukuru msaada mkubwa wa Shirika la Uswisi la Maendeleo na Ushirikiano (SDC). Maoni yaliyotolewa kwenye ripoti hii ni ya waandishi na si lazima yaakisi sera rasmi au msimamo wa SDC.

Tunatoa shukurani pia kwa michango mingi iliyotolewa na timu ya utafiti, ambayo ilikuwa na watu wafuatao:

| | |
|---|---|
| Julie Bwire | Mkulima kinara (Mvomero) |
| Mathias Daud | Kilimo Endelevu Tanzania |
| Abdallah Ibrahim | Mkulima kinara (Mvomero) |
| Gareth Jones | Kituo cha Afrika cha Bioanuwai |
| Stanslaus Kissatu | Kilimo Endelevu Tanzania |
| Janet Maro | Kilimo Endelevu Tanzania |
| Japhet Masigo | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania |
| Sabrina Masinjila | Kituo cha Afrika cha Bioanuwai |
| Amina Mwaibula | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania |
| Meddy Njusi | Kilimo Endelevu Tanzania |
| Pius Paulini | Mkulima aliyesaidia (Morogoro) |

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| ACB | Kituo cha Afrika cha Bioanuwai |
| CSO | Asasi ya Kiraia |
| FGD | Majadiliano ya vikundi |
| FMSS | Mfumo wa mbegu unaosimamiwa na mkulima |
| MVIWATA | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania |
| OPV | Aina za Mbegu Zilizopevushwa Kiasili |
| QDS | Mbegu Zilizothibitishwa Ubora |
| R&D | Utafiti na Maendeleo |
| SAT | Kilimo Endelevu Tanzania |
| SSA | Afrika Kusini mwa Sahara |
| SUA | Chuo Kikuu cha Kilimo, Sokoine |
| TOAM | Asasi ya Kilimo Hai Tanzania |
| VBAA | Mshauri wa Kilimo Kijijini |

# Utangulizi

Mfumo wa mbegu unaosimamiwa na mkulima (FMSS) ndio msingi imara wa maisha ya vijijini na uzalishaji katika kilimo nchini Tanzania. Wakati ukweli huu ukitambuliwa na wadau wengi katika sekta ya kilimo, ikiwa pamoja na wakulima wadogo wenyewe, mfumo huu hauungwi mkono na mazingira ya sera ambayo yametawaliwa na msisitizo kwenye mbegu zilizothibitishwa/bora na tija.

Ripoti hii kutoka maeneo mbalimbali inashirikishana matokeo ya kazi za mashambani zilizofanyika katika wilaya za Morogoro na Mvomero mwaka 2016. Ni mwendelezo wa ubia baina ya Kituo cha Afrika cha Bioanuwai (ACB), Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) na Kilimo Endelevu Tanzania (SAT). Ubia ulilenga kwenye masuala yanayohusiana na mbegu, hususani Mfumo wa mbegu unaosimamiwa na mkulima.

Malengo ya utafiti ni pamoja na: kubaini mazao na aina zake yanayotumika katika maeneo ya utafiti, kuainisha miradi au programu za sasa na zilizopita zilizolenga katika kukuza Mfumo wa mbegu unaosimamiwa na mkulima (FMSS) katika maeneo haya; kubaini wakulima, mashirika au taasisi katika maeneo hayo ambayo yanapenda kusaidia kuendeleza kazi kwenye mfumo wa FMSS. Utafiti unalenga katika kufanya matayarisho kwa ajili ya shughuli za vitendo pamoja na wakulima, mashirika wabia na taasisi za sekta binafsi, kuwezesha kazi zao kwenye maeneo ya kipaumbele ya FMSS kama yalivyoainishwa na wakulima washiriki. Lengo ni kujenga shughuli za utafiti za miaka mingi ambazo zitaweza kutoa msaada wa vifaa kwa wakulima, hususani kukuza aina zao za mbegu na kusaidia vipengele vingine vya mfumo wa mbegu, kulingana na vipaumbele vilivyoainishwa.

## Mbinu Za Utafiti Na Historia Fupi Ya Maeneo Ya Utafiti

Mzunguko huu wa utafiti ulijumuisha wawakilishi wa wakulima pamoja na wengine waliounda timu ya utafiti kutoka wilaya za Morogoro na Mvomero. Wawakilishi wa wakulima walijitolea kikamilifu katika mchakato mzima na waliongeza thamani kubwa katika majadiliano wakati wa mahojiano na watoa taarifa muhimu na ziara za mashambani.

Tuliendesha jumla ya majadiliano tisa ya vikundi (FGDs) (4 katika wilaya ya Mvomero 5 wilayani Morogoro) na wakulima na Washauri wa Kilimo wa Vijijini, pakiwa na wahojiwa 10–12 katika kila kikundi. Jumla ya wakulima 82 walishiriki katika Majadiliano ya Vikundi —42 kutoka Morogoro na 40 kutoka Mvomero. Majadiliano ya Vikundi yalitenganishwa katika makundi ya jinsia na umri: palikuwepo na makundi mawili ya vijana (kwa wakulima chini ya miaka 35), makundi mawili ya wanawake pekee, makundi mawili ya wazee pekee (kwa wakulima wenye umri zaidi ya miaka 50) na kundi moja mchanganyiko. Kuundwa kwa makundi haya kulilenga kupata maoni anuwai kuhusu uendeshaji na umuhimu wa mfumo wa FMSS kutoka kwenye vikundi tofauti. Wakulima hawa walitoka vijiji vya Mkindo, Msufini, Hembeti, Kigugu, Dihombo na Mbogo katika wilaya ya Mvomero; na pia kutoka vijiji vya Kiroka, Soweto, Kenge na Towelo katika wilaya za Morogoro na Morogoro Vijijini.

Mahojiano na watoa taarifa muhimu yaliendeshwa na wafuatao: Dk. Sophia Kashenga-Killenga, Afisa Mtafiti Mkuu wa Kilimo na Mzalishaji wa Zao la Mpunga kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Dakawa; Moses Temi, Mkuu wa Kituo cha Mafunzo, Mkindo; Profesa Joseph Hella kutoka SUA,[1] maafisa ugani wa vijiji katika wilaya ya Mvomero, msaga nafaka/mkulima, mzalishaji wa mbegu, wafanya biashara ya nafaka/mbegu katika soko la eneo na maafisa kilimo kutoka SAT. Ziara shambani kwa mkulima ambazo zilitumika kama mashamba darasa kwa wakulima (FFS) zilishamirisha mahojiano muhimu ya watoa taarifa na Majadiliano ya Vikundi. Aidha, kwa sababu masoko ni chanzo muhimu cha nafaka na mbegu, timu ya utafiti ilitembelea masoko sita yaliyopo katika maeneo ya mkoa wa Morogoro.

1. Profesa Hella alikuwa mtunzi mkuu wa wasilisho lililotolewa na TOAM mwaka 2015, limaloitwa 'Mifumo ya Mbegu Inayosimamiwa na Mkulima nchini Tanzania'.

# Mazao Na Aina Za Mbegu Zinazotumika Katika Maeneo Ya Mvomero Na Morogoro

Urafiti uliofanyika katika wilaya za Morogoro na Mvomero uligundua kwamba kuna aina za mazao na mbegu zinazooteshwa na kutumika, na kuandika aina 91 tofauti za mazao, mimea ya porini na miti. Wakulima wadogo waliorodhesha aina 20 za mchele, chakula kikuu katika eneo hilo, kati ya hizo 17 ni aina za mkulima. Mahindi lilikuwa zao pekee ambalo aina za mbegu zilizothibitishwa zilikuwa zaidi ya aina za mkulima. Aidha, iligundulika kwamba miti na mimea mbalimbali ya porini inatumika kwa ajili ya dawa, ikijumuisha tiba ya malaria, shinikizo la damu na maambukizi ya minyoo, pia kama viuatilifu vya kibailojia. Ijapokuwa miti na mimea ya porini inapatikana kwa urahisi, upatikanaji wake unadhibitiwa, na kuna maelewano ya wazi na yasiyo wazi miongoni mwa wakulima kuhusu uvunaji wa busara wa rasilimali hizi.

**Jedwali 1: Orodha ya mazao yanayopandwa katika maeneo ya Morogoro na Mvomero**

| Aina ya Mazao | Idadi |
|---|---|
| Nafaka | 4 |
| Mazao ya mizizi na viungo | 5 |
| Mazao ya mikunde | 3 |
| Mazao ya mafuta | 3 |
| Mbogamboga | 15 |
| Matunda | 14 |
| Miti na mimea ya dawa | 47 |
| **Jumla** | **91** |

**Jedwali 2: Aina za mazao ya nafaka, mikunde, mboga mboga yanayotokana na mkulima na yaliyothibitishwa**

| Mazao | Aina za mbegu za Mkulima | Aina za Mbegu Zilizopevushwa Kiasili | Chotara |
|---|---|---|---|
| Mchele (mpunga) | Supa Shinyanga, Supa India, Supa Mbeya, Supa Ifakara, Mbawa mbili, Rangi mbili, Shingo ya Mwari, Domo la Fisi, Moshi wa Taa, Kihogo, Tule na bwana, Mwarabu, Nondo, Shingo ya kuku, Cheza, Seselolunyukwi, Sindano, Meli nyeupe, Kongo, Karafuu | Supa, TXD 306 (Saro 5), Nerica | |
| Mahindi | Katu mbili, Plenda*, Ilonga Kito, Kitweeko, Mhingo, Manjano, Kimekele, White Tango, Colman, Kihingo* | Staha, Ilonga, Katumani, TMV1, NATA, MMCLU, Situka, TAN 254, TAN H 600, TAN 236 | Pannar, SeedCo, Kifaru |
| Mtama | Kalashi, Kibangala | | |
| Uwele | Mdeha* | | |
| Muhogo | Manyanga, Kibanga meno, Moshi wa taa, Kibanga meno | Muhogo | |
| Viazi vitamu | Bwarabwara* | Viazi vitamu | |
| Kunde | Kisasamali, Luswaluswa | | |
| Mbaazi | Balongo, Pombwe, Kwazu | | |
| Maharage | Machale, Gololi, Kombati, Kisengo*, Kasafaringo | | |
| Soya | Mfawima, Gairo, Njano | | |
| Nyanya | Tonogwe | Asilla | |
| (Mchicha) | Bwasi, Mchicha Mweupe, Mchicha chakaya | Mchicha lishe | |

*Aina zilizopotea/zinazopotea

Matokeo ambayo yameleta wasiwasi ni mwelekeo dhahiri wa kupotea kwa aina za mbegu za kienyeji. Hii inatokana na magonjwa ya mimea, au shinikizo walilo nalo wakulima kuacha kuzitumia, au zinapobadilishwa na aina ya mbegu zilizothibitishwa na zilizo na ruzuku. Idadi kadhaa ya aina za mbegu za kienyeji za mahindi, mbaazi, uwele, mpunga na maharage zinasemekana hazipatikani tena kwenye eneo hilo. Katika maeneo ya milimani, aina za kienyeji za muhogo na viazi vitamu pia zinapotea kutokana na kukabiliwa na magonjwa. Kuhusiana na mazao ambayo si ya biashara—uwele, mbaazi, muhogo na viazi vitamu—ni jambo linalotia hofu kubwa, kwani kuna uwekezaji mdogo wa utafiti katika mazao haya. Upotevu huu wa bioanuwai ya kilimo una athari za moja kwa moja za kupunguza anuwai za lishe katika maeneo haya.

Ijapokuwa maarifa kuhusu aina hizi zimerithishwa kwa vizazi na vizazi hakuna mfumo mzuri wa uwekaji wa kumbukumbu ya habari hizi. Upungufu huu wa kumbukumbu za kihistoria katika kilimo una hatari ya kupotea kwa mengi ya maarifa haya katika haraka za Tanzania ya kufanya kilimo chake kuwa cha kisasa. Majadiliano yetu na wakulima yamefichua mgawanyiko dhahiri kati ya vizazi vya kale na sasa katika maarifa yaliyopo kuhusiana aina za mazao ya kienyeji na mimea na miti pori ya dawa.

Hakuna shaka kwamba mabadiliko ya kijamii na kiuchumi katika ngazi za juu, yaliyoambatana na msisitizo dhahiri kwenye mbegu zilizothibitishwa na tija katika vituo vyetu vya mafunzo na programu za kilimo, ndio visababishi vikuu vinavyofanya hali kuwa hivi. Kuna hatari ya kweli kwamba mengi ya maarifa haya yatapotea iwapo sera na motisha katika ngazi za vijiji na kitaifa hazitawekwa, hivi karibuni, kulinda maarifa ya asili. Hii itahitaji pawepo na ari ya kisiasa pamoja na msaada wa kitaalamu. Licha ya idadi kubwa ya aina za mazao za wakulima zilizotamkwa, hasa na wakulima wazee, nyingi kati ya hizi hazioteshwi tena, hivyo kuaminika zimepotea.

Wakulima walionyesha wasiwasi kwamba kama aina zao za kienyeji hazitapewa thamani kubwa, na sekta ya umma, basi aina nyingi zaidi zitabadilishwa na aina zilizothibitishwa zilizo ghali zaidi. Katika wilaya ya Mvomero wakulima vinara walisadiki kwamba wanaweza kufufua mbegu zao za kienyeji kwenye mashamba yao. Hata hivyo, mpango huu utategemea pia ari ya wakulima wengine, maafisa ugani na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi katika maeneo yao, kusaidia vikundi hivi vya wakulima.

### Sifa Muhimu Za Mbegu Za Kienyeji

Licha ya kukosolewa siku zote na wafadhili, watunga sera na wazalishaji wa mimea kwamba aina za mbegu za wakulima ni za viwango duni na zimepitwa na wakati, wakulima wadogo walioshiriki katika utafiti huu walipendelea mbegu za kienyeji, kwa sababu za kitamaduni pamoja na za kiuchumi. Walitaja vipengele kama vile gharama, urahisi wa kupatikana, sifa za ladha na harufu nzuri na uhimilivu mzuri dhidi ya wadudu waharibifu, kama baadhi ya faida zilizo kwenye mbegu za kienyeji ukilinganisha na mbegu zilizothibitishwa.

Wakulima walionyesha kwamba aina za mpunga wa kienyeji zinavumilia zaidi ukame na zinahitaji maji kidogo ukilinganisha na mbegu za kisasa. Hata hivyo, iwapo mbegu za kisasa zinazokomaa mapema zikitumika katika skimu za umwagiliaji, wakulima wanaweza kulima si chini ya mara mbili kwa mwaka, wakati mbegu za kienyeji kwenye mashamba ya kawaida huchukua miezi 6–7 kukomaa.

Mbegu za kisasa za mahindi hazichukui zaidi ya miezi mitatu hadi kuvuna, wakati mbegu za kienyeji za wakulima huchukua si chini ya miezi sita kukomaa. Kuna hatari kubwa ya kukosa mavuno ya mahindi unapopanda mbegu za kienyeji, ukilinganisha na mbegu za kisasa. Mbegu Zilizopevushwa Kiasili za mahindi kama vile Staha zinapendwa kwa vile zinahimili ukame na hazishambuliwi kirahisi na wadudu zinapohifadhiwa.

Jinsi jinsia zinavyochagua, pia huamua aina ya mazao yatakayopandwa.

Magonjwa hufikiriwa kuwa tatizo kubwa kwa mbegu za kienyeji, wakati wadudu waharibifu ni tatizo kubwa kwa mbegu za kisasa. Wakulima walisema kwa ujumla mbegu za kisasa hushambuliwa kwa urahisi zaidi na wadudu waharibifu, mazao yakiwa shambani na ghalani baada ya kuvuna.

# Huduma Za Ugani Na Maarifa Ya Aina Za Mbegu Za Mkulima

Nchini Tanzania huduma za ugani za umma katika kilimo hutekeleza jukumu muhimu katika kutoa habari na mafunzo kwa wakulima, na katika kueneza habari baina ya ngazi mbalimbali za serikali za mitaa, mkoa na kitaifa.

Maeneo ambayo utafiti wetu ulifanyika yanaonekana kuwa na huduma za ugani zilizojiimarisha vyema na kufanya kazi ambazo, pamoja na majukumu mengine mengi, hufanya kazi kama njia kuu za kujifunza na kushirikishana habari baina ya wakulima na sekta ya umma. Pia, idara ya utafiti na maendeleo ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Dakawa, hutoa msaada wa kitaalamu kwa wakulima na kuna mtandao mzuri unaofanya kazi wa Washauri wa Kilimo wa Vijijini pamoja na mashamba darasa. Pamoja na vipengele hivi chanya, mazingira ya sera yanajenga mfumo wa kuunga mkono mbegu bora/zilizothibitishwa na kutojali mbegu za wakulima, na mfumo mzima wa utafiti na maendeleo, na ugani unakuwa mkondo wa mbegu za kisasa. Hata hivyo, mfumo huo huo wa kitaasisi unaweza kirahisi kurekebishwa kwa ajili kufanya majaribio shirikishi kwenye mbegu za wakulima—na kuna hamasa kubwa katika kuchunguza njia hiyo. Wakulima wanatoa wito kwa huduma za ugani wa kilimo, kuelekeza juhudi zaidi katika Mfumo wa Mbegu Unaosimamiwa na Mkulima (FMSS) kwa utaratibu mzuri, na mfumo wa umma wa utafiti hutoa fursa ya kuanzishwa kwa mahusiano ya kikazi na wakulima katika uchaguzi shirikishi wa aina za mbegu, na kujenga mbegu bora za kienyeji. Cha kusikitisha, shughuli hizo hazina ufadhili.

Katika skimu za umwagiliaji, kwa mfano, maafisa ugani husisitiza matumizi ya mbegu za kisasa na sio za kienyeji, licha ya matumizi yaliyoenea ya mbegu za kienyeji. Maafisa ugani walio na umri mkubwa huonyesha kiwango fulani cha maarifa na uzoefu kuhusu maarifa ya wenyeji, lakini sera inaamuru nini wafundishe katika vyuo vya wakulima, na wanakatazwa kushauri wakulima kuhusu hizi zinazoitwa 'teknolojia zilizopitwa na wakati'.

# Kupata Mbegu

Mbegu zilizohifadhiwa kutoka shambani au za kubadilishana, na kwenye masoko ya vijiji ndio vilikuwa vyanzo vikuu vya mbegu kwa wakulima walioshiriki katika utafiti huu. Unapotembelea masoko ya maeneo mbalimbali yanaonyesha biashara ya mbegu iliyoshamiri katika aina mbalimbali za mchele, mahindi, maharage, mtama, bamia na haibiskasi, kwa kutaja aina chache tu. Mbali na gharama na upatikanaji, wakulima vijijini wanaponunua mbegu huwaamini zaidi majirani, au wafanyabiashara sokoni wanaofahamika (ambao wengi wao pia ni wakulima), kuliko wasambazaji mahususi wa pembejeo. Lakini, kwa kufanya hivyo, wakulima na wafanya biashara wanachukuliwa kuwa wanajihusisha na shughuli haramu—kwa sababu sheria za mbegu za Tanzania zinazuia kuuza mbegu zisizothibitishwa. Tofauti na hali halisi inayowakabili wakulima wadogo kila siku, sheria za nchi za sasa zinashurutisha viwango vya nje visivyo sahihi katika ubora na uthibitisho wa mbegu.

Miaka ya nyuma, wakulima nchini Tanzania walichangia mbegu kwa chifu wao wa kijiji au jumbe inapofika mwishoni mwa kila msimu, ambazo zilihifadhiwa katika ghala la dharura. Utamaduni huu unapotea na, ijapokuwa akiba za mbegu za jamii bado zipo katika maeneo machache, utamaduni huu haujabadilishwa na njia nyingine mbadala. Wakulima wengi wadogo wanachukulia kwamba shughuli zao za kuhifadhi na kubadilishana mbegu hujenga akiba hai ya mbegu ya jamii, na palikuwepo na makubaliano kwamba juhudi hizi ziungwe mkono rasmi na serikali.

Wakulima walitaja njia mbalimbali za uhifadhi, zinazojumuisha maghala ya kienyeji, mifuko maalumu ya plastiki kuhifadhia mazao inayojulikana kama Purdu, mapipa ya chuma kwenye dari na/au jikoni, ambako moshi unatumika kuhifadhi mbegu na kuzuia mashabulizi ya wadudu waharibifu na magonjwa.

## Uchaguzi Na Uzalishaji Wa Mbegu

Mfumo wa Mbegu Zilizothibitishwa Ubora (QDS) hufanya kazi na unatambulika kisheria nchini Tanzania. Majadiliano yamefanyika baina ya maafisa wa serikali, wakulima na asasi za kiraia (AZAKi), kupanua wigo wa maeneo ya Mfumo wa Mbegu Zilizothibitishwa Ubora, lakini jambo hili limekosolewa na sekta binafsi na baadhi ya sekta za umma.

Katika wilaya ya Morogoro wafanyakazi wa shirika la SAT vijijini walizungumza na baadhi ya wakulima waliokuwa wanazalisha mbegu kwa ajili ya kuzisambaza, ambazo ni pamoja na maharage, mchicha, mtunguja na mbegu nyingine za wenyeji. Kwa sehemu kubwa wazalishaji hawa wa mbegu walikuwa wanafanya hivyo bila ya msaada wowote au mafunzo rasmi, lakini bado mbegu zao zilipendwa sana na wenyeji. Katika wilaya ya Mvomero tulizungumza na mkulima, Bw. Sadick Mohammed, ambaye hapo awali alikuwa anazalisha mbegu ya mahindi ya kienyeji, kwa kipindi cha takribani miaka 20, hadi miaka ya 1990 katikati. Wakati akifanya kazi katika kituo cha utafiti wilayani Bagamoyo, Bw. Mohammed alipata mafunzo ya ziada katika uzalishaji wa mbegu, na alitumia ujuzi huu kwenye kijiji chake, akizalisha aina za mbegu za mahindi ya kienyeji - Kile na Kitweko (hii aina ya pili inabainishwa kwa kokwa za rangi ya zambarau na nyeupe).

Bw. Mohammed anaelezea jinsi alivyochagua mbegu za mahindi, kwa kuchagua kutoka kwenye magunzi yenye rangi sawa pekee, akichukua katikati ya gunzi ambapo kokwa ni kubwa zaidi. Ili kuhakikisha aina za mbegu zilizo safi kwa kuepuka uchavushaji mtambuko na aina nyingine, mbegu zilichukuliwa kutoka katikati ya shamba. Bw. Mohammed alieleza kwamba umbali wa mita 200 ni muhimu sana kuhakikisha usafi wa aina ya mbegu, na kwamba hapo awali, wakati alipokuwa anamiliki eka 8 (takribani hekta 3.2) za ardhi, aliweza kulima mahindi kulingana na umbali wa kutenganisha uliopendekezwa. Hata hivyo, kwa sasa kama ilivyo kawaida katika maeneo ya Morogoro na Mvomero, anamiliki eka 2 au 3 tu (hekta 0.8–1.2), ambazo hazitoshi kwa ajili ya kujishughulisha katika uzalishaji wa mbegu. Sababu hii, pamoja na mifumo ya hali ya hewa isiyotabirika, ndio sababu kuu kwa nini Bw. Mohammed hazalishi tena mbegu.

Palikuwepo na makubaliano ya jumla miongoni mwa wajumbe wenyeji wa timu ya kitaalamu kwamba kuanzishwa kwa wazalishaji wa mbegu za kienyeji, kutakuwa na manufaa makubwa, kwani 'ubora wa mbegu za mahindi umepungua'. Lakini mafanikio ya mbinu hii yatahitaji upatikanaji mzuri wa mbegu za kienyeji zilizo safi, ambapo kwa sasa aina nyingi za kienyeji zinazotumika hufikiriwa kwamba sio safi (au zenye sifa zote za aina hiyo).

Wakulima vijana walizungumzia mchakato tofauti wa kuchagua mbegu za mpunga, ambao hufanyika wakati wa msimu wa kupanda, na wakaonyesha kwamba walijifunza mbinu hiyo katika Kituo cha Mafunzo cha Mkindo. Mbegu za mpunga zinawekwa kwenye chombo chenye maji ya chumvi na kuachwa zielee; mbegu zinazoelea zinaondolewa; mbegu zinazozama hadi chini ya chombo husuuzwa vizuri katika maji safi na baadaye kukaushwa au kupandwa mara moja. Mbinu inayofanana na hii imeelezwa kikamilifu katika ripoti kuhusu FMSS iliyotolewa na TOAM (2015).

Wanawake wanaonekana kujihusisha zaidi katika kuvuna na kuhifadhi mbegu, lakini hii inatofautiana kutegemea na aina ya zao na matumizi yake.

## Matumizi Na Usindikaji

Upendeleo wa wakulima kuhusiana na ladha na harufu nzuri ya mazao ya kienyeji hauwezi kupuuzwa. Aina za kienyeji mara nyingi hupendwa na wakulima, wafanyabiashara na walaji—zina aina zote za vipengele muhimu (harufu na ladha) na pia ni nzuri kwa usindikaji.

Kuhusiana na kukoboa aina za mpunga kwenye mashine za kukoboa, wafanya biashara hupendelea Mbawa mbili—inatakiwa sana, ina harufu nzuri na punje zake hazikatiki wakati wa kukoboa. Hata hivyo, wakoboaji wanaweza kupata kilo chache za aina ya mpunga wa kienyeji kutoka kwa wakulima, kutokana na mavuno kidogo na inawabidi walipie zaidi kwa ajili ya aina za kienyeji, kuliko kwa aina za kisasa.

# Hitimisho Na Hatua Zinazofuata

Utafiti huu ulikuwa hatua ya kwanza katika mchakato wa kutambua aina za mbegu wanazotumia wakulima, iwapo mbegu hizi zinafaa kwa mahitaji yao, ni maboresho gani wakulima wanapenda, na iwapo wakulima wanapenda kuendeleza suala hilo, kwa ubia na Kituo cha Afrika cha Bioanuwai (ACB), MVIWATA na Kilimo Endelevu Tanzania (SAT).

Kuhusiana na uwezekano wa kufanya maboresho katika aina za mbegu wanazotumia wakulima, vipaumbele vya juu ni mavuno mengi na muda mfupi wa kukomaa, wakati zikibaki na sifa chanya za aina za kienyeji. Taratibu za kitaasisi kwa ajili ya maboresho kwa sehemu kubwa zimewekwa. Hizi ni pamoja na huduma ya ugani inayofanya kazi, muundo wa Washauri wa Kilimo Vijijini na mashamba darasa, na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Dakawa na Kituo cha Mafunzo cha Mkindo, ambavyo hupatikana kwa ajili ya kutoa ushauri wa kitaalamu. Huduma ya ugani, MVIWATA na SAT hufanya kazi kama asasi za kiraia. Ijapokuwa sera inaelekeza katika kuhimiza kuendeleza na matumizi ya aina za mbegu zilizothibitishwa, kuna shauku miongoni mwa watendaji hawa kufanyia kazi aina za mbegu wanazotumia wakulima kwa njia shirikishi.

Wakulima na watoa habari muhimu walioshiriki katika utafiti huu kwa ujumla walikuwa na mtazamo chanya sana kuhusu fursa ya mahusiano ya moja kwa moja baina yao na kwa utaratibu wa kawaida. Umuhimu wa kuwapo kwa mahusiano ya kazi endelevu na ya muda mrefu baina ya wakulima na mashirika yanayowapa misaada hauwezi kusisitizwa zaidi.

Wakulima walionyesha hamu ya msaada zaidi kutoka kwa maafisa ugani, hususani kwa aina za mbegu wanazotumia wakulima, na pia walifanya maombi ya wazi kwa ajili ya mafunzo ya ziada kuhusu udhibiti wa magonjwa ya mimea kwa ajili ya mazao yanayozalishwa kwa kupandikizwa, na kupima udongo. Wakulima kubadilishana na kushirikishana maarifa mahususi kwa maeneo yao kuhusu aina za mbegu wanazotumia wakulima na mimea ya porini lilianishwa kama eneo lenye maslahi. Wito ulitolewa kwa ajili ya kuongeza utafiti katika kuboresha aina za mbegu wanazotumia wakulima na katika kutoa msaada kwa wakulima wanaotaka kuanzisha uzalishaji wa aina za mbegu za kienyeji.

Hatua zinazofuata zitakuwa kushirikishana matokeo ya utafiti huu na washiriki, na baadaye kujadili njia za kufanya ili kuendeleza kazi hii. Hizi zinaweza kujumuisha utambuzi wa watu mahususi ambao wanapenda kufanya majaribio na aina za mbegu wanazotumia wakulima; kuainisha aina mahususi na kukuza /maboresho wanayopenda kufanya; kuwezesha majadiliano na wakulima kuhusu jinsi ya kuhakikisha wanabaki na udhibiti juu ya mbegu zozote za kisasa; majadiliano kuhusu viwango vya ubora katika ngazi ya kijiji na wakulima na wataalamu; na kuwahusisha wataalamu na huduma za ugani kuona jinsi gani michakato hii inaweza kuanzishwa. Kutakuwa pia na fursa ya kuchunguza kwa kina vipengele vingine vya mifumo ya mbegu za wakulima, pamoja na wakulima.

Licha ya kuwa mbali na uwanja wa sera, kwa uhalisia na kifikra, wakulima wengi wanatambua kwamba mazingira ya sasa ya sera yako mbali na kuwa rafiki na shughuli zao za kilimo. Wamependekeza kufanyike marekebisho kwenye sheria za mbegu ili kufanya sheria hizi kuwa sikivu zaidi kwa uzoefu wao wa kila siku wa kilimo, pia wametoa wito wa kubadilishwa kwa ruzuku, kutoka mbegu chotara na mbolea, kwenda aina za mbegu wanazotumia wakulima.

african centre for biodiversity

PO Box 29170, Melville 2109, South Africa
www.acbio.org.za